
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA WA FEDHA 2018/19 KWA LUGHA RAHISI

## Toleo la Wananchi




Imetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango
kwa kushirikiana na Policy Forum


policy forum

# 1. UTANGULIZI

**Bajeti Toleo la Wananchi** ni toleo linaloandaliwa kila mwaka wa fedha ili kutoa taarifa za msingi za Bajeti ya Serikali kwa wananchi kwa lugha rahisi.Toleo hili limekuwa likiandaliwa tangu mwaka wa fedha 2010/11 kwa lengo la kuwawezesha Wananchi kufahamu Mipango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha husika, pia kuwapa mwanga wa jinsi ya kushiriki katika mipango na bajeti ya Serikali. Bajeti Toleo la Wananchi la mwaka wa fedha 2018/19 linaanza na utangulizi unaojumuisha dhana ya bajeti kwa ujumla, mchakato wa bajeti na malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19. Maeneo mengine yanayofuata yanahusu: Vipaumbele vya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19; Sera na hatua muhimu za kuiwezesha bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19; Maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbali mbali; Namna Serikali itakavyopata fedha; na Jinsi Serikali inavyotarajia kutumia fedha.

**Bajeti ya Serikali ni nini?** Ni mpango wa Serikali unaoelezea jinsi mapato yatakavyopatikana na jinsi Serikali itakavyotumia mapato hayo kwa mwaka mmoja. Bajeti hutumiwa na Serikali kama nyenzo ya kutafsiri sera zake na kuainisha mgawanyo wa rasilimali zilizopo na jinsi zitakavyotumika kutekeleza sera na vipaumbele vya Taifa kwa mwaka husika. Bajeti ya Serikali huandaliwa na kuwasilishwa bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015.

**Mchakato wa Bajeti ya Serikali:** Maandalizi ya bajeti huanza kwa Serikali kutoa Mwongozo wa Mpango na Bajeti unaotoa vipaumbele na maelekezo ya uandaaji wa Bajeti kwa mwaka husika. Aidha, Serikali hupokea mahitaji mbalimbali kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri) yanayoendana na rasilimali fedha zinazotarajiwa kukusanywa na kuyajumuisha pamoja. Baada ya maandalizi bajeti huwasilishwa kwenye hatua mbalimbali za uidhinishwaji ikiwa ni pamoja na Baraza la Mawaziri na hatimaye Bunge. Bajeti ikishaidhinishwa na Bunge huanza kutekelezwa ikifuatiwa na ufuatiliaji unaoendana na utoaji wa taarifa za mapato na matumizi ili kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kwa ufanisi. Kwa ujumla, mchakato wa bajeti hupitia hatua kuu nne ambazo ni: ***Uandaaji, Uidhinishwaji, Utekelezaji na Ufuatiliaji.***



**Malengo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19:** Malengo makuu ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 ni kupambana na umaskini na kuiwezeshaTanzania kufikia uchumi wa viwanda wa kipato cha kati. Malengo haya yanaendana na yale ya: Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21), Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030) na Ilani ya CCM (2015 – 2020). Hivyo, kauli mbiu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 ni **"Kujenga uchumi wa viwanda utakao chochea ajira na ustawi endelevu wa jamii**".

# 2. VIPAUMBELE VYA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2018/19, Bajeti ya Serikali imeweka mkazo zaidi katika uendelezaji wa miradi ya kielelezo[1]; Kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu; na Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji na uendeshaji biashara. Hivyo, maeneo ya kipaumbele yatakuwa:

**a) Kilimo:** Sekta hii inategemewa na wananchi wengi katika kupata mazao ya chakula na biashara, kuongeza kipato pamoja na kuzalisha malighafi za viwanda. Bajeti inalenga:

i. Kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, maghala na masoko na kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo, kupanua huduma za ugani;

ii. Kuboresha utafiti wa kilimo na mbegu bora pamoja na utoaji wa matokeo ya utafiti ambayo yatalenga kutatua matatizo ya wakulima na sekta ndogo za uvuvi na mifugo.

b) **Viwanda:** Bajeti inalenga kuboresha mazingira na usimamizi wa uwekezaji wa sekta binafsi hasusani viwanda vya nguo, ngozi, nyama, samaki, mafuta ya kula, madawa na vifaa tiba, vyakula vya binadamu na mifugo na katika sekta ya madini.

c) **Huduma za Kijamii**: Bajeti imelenga kuboresha huduma za kijamii katika maeneo yafuatayo:

⇨ ***Maji***

i. Kuongeza upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama hasusan vijijini na uondoshaji wa maji taka katika maeneo ya makazi;

[1] **Miradi ya Kielelezo** ni miradi itakayochochea ukuaji wa sekta mbalimbali na hivyo kuchochea uchumi kwa haraka, ambayo ni pamoja na: Ujenzi wa reli ya kati, Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania, Kuzalisha Umeme kwa maji bonde la mto Rufiji, Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma, Kiwanda cha kufua chuma cha Liganga, Shamba la miwa na kiwanda cha sukari Mkulazi, Uanzishwaji wa kanda maalumu za kiuchumi (EPZ), Uchakataji na usindikaji gesi asilia,

i. Uchimbaji wa visima katika maeneo kame na ujenzi wa mabwawa makubwa ya kimkakati2.

⇨ ***Elimu***

Kugharamia Elimu Msingi bila Ada (darasa la awali mpaka kidato cha nne), kuongeza idadi ya wataalamu katika fani adimu kwenye maeneo ya madini, mafuta na gesi, madaktari bingwa na kuongeza utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

⇨ ***Afya***

i. Upatikanaji na usambazaji wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na uboreshaji wa huduma katika vituo vya afya, zahanati na hospitali za rufaa;
ii. Kuelekeza ruzuku ya afya kwenye miradi ya maendeleo ya Halmashauri, sekta ya afya;
ii. Kuimarisha upatikanaji wa lishe bora kwa mama na mtoto ili kuwezesha mtoto kukua vyema kimwili, kiakili na kuepusha watoto wenye udumavu;
**iii.** Kuangalia mahitaji ya makundi maalumu katika jamii hususan wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wazee.

**d) Miundombinu wezeshi:** Kujenga na kukarabati miundombinu wezeshi kama ifuatavyo:

i. Uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali;
ii. Kuendeleza ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge);
iii. Ujenzi wa barabara za kuunganisha mikoa na zile za vijijini; na
iv. Kuimarisha usafiri wa anga na majini.




[2] **Mabwawa ya Kimkakati** ni mabwawa ya maji kwa lengo maalum ambayo yanajumuisha bwawa la Farkwa, Lugoda/Ndembera, Kidunda na Songwe.

# 3. SERA NA HATUA MUHIMU ZA KUIWEZESHA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/19

### Matarajio Katika Ukuaji wa Uchumi na Misingi ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19

Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 inalenga kufikia baadhi ya shabaha za uchumi jumla kama ifuatavyo:

a. Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 kwa mwaka 2018 kutoka ukuaji wa asilimia 7.1 mwaka 2017;
b. Kuthibiti mfumuko wa bei kubaki katika wigo wa tarakimu moja;
c. Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya pato la taifa kwa mwaka wa fedha 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 15.3 kwa mwaka wa fedha 2017/18;
d. Nakisi[3] ya bajeti kufikia asilimia 3.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/19;
e. Akiba ya fedha za kigeni yenye kukidhi uingizaji wa bidhaa za nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Ili kufikia shabaha na malengo yaliyokusudiwa, misingi wezeshi inayotarajiwa ni:

a. Amani, umoja, utulivu wa kisiasa ndani ya nchi na katika kanda;
b. Kutengamaa na uendelevu wa viashiria vya uchumi jumla (ikijumuisha ukuaji wa pato la taifa, biashara ya nje, ukusanyaji wa mapato ya ndani);
c. Kutengamaa kwa uchumi wa dunia;
d. Kutengamaa kwa bei za mafuta ya petrol kwenye soko la dunia;
e. Hali nzuri ya hewa nchini na katika nchi za jirani;
f. Uhusiano mzuri na nchi jirani, kikanda na kimataifa; na
g. Kuwepo kwa sheria na kanuni wezeshi kwa wawekezaji.

### Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato

Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 itaendelea kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuzingatia hatua za kiutawala zifuatazo:

a. Kuanzisha Akaunti Jumuifu ya Hazina itakayotumika kupokea fedha zote za Serikali na kufanya malipo yote ya Serikali ili kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na kupunguza gharama za kibenki;
b. Ushuru unaokusanywa na Bodi za mazao mbalimbali kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kuwa mapato hayo yanasimamiwa na kutumika ipasavyo;

[3] **Nakisi ya bajeti** ni pengo kati ya kiasi kinachotarajiwa na kinachopatikana katika kipindi husika.

c. Kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya mapato vilivyopo hususani katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki;
d. Kuongeza wigo wa kodi kwa kurasimisha sekta isiyo rasmi;
e. Kuboresha mazingira ya uwekezaji na urasimishaji ili kuvutia biashara na uwekezaji ikiwemo: Kuboresha miundombinu; Vivutio vya kodi; Sera thabiti zisizobadilika mara kwa mara; Upatikanaji wa ardhi; na Uwepo wa taratibu za kisheria na usimamizi bora.
f. Kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo.




### Sera na Hatua za Kusimamia Matumizi

Sera za matumizi katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 zinajumuisha:

a. Kudhibiti nakisi ya bajeti isizidi asilimia 3.2 ya Pato la Taifa;
b. Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele na yenye tija ili: Kuchochea ukuaji wa kilimo na viwanda; Kupanua fursa za ajira; Kujenga na kuboresha miundombinu ya uchumi; na Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za jamii;
c. Kusimamia nidhamu na matumizi ya fedha za umma na kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima; na
d. Kudhibiti ulimbikizaji wa madeni.

Katika kusimamia sera za matumizi, hatua zifuatazo zitachukuliwa:


i. Hatua za kisheria, kiutawala na kinidhamu kwa watakaothibitika kwenda kinyume na sheria na kanuni zinazoongoza utendaji katika taasisi zao;
ii. Maafisa Masuuli (waidhinishaji wa fedha) kutoingia mikataba bila kuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha au ridhaa ya Mlipaji Mkuu wa Serikali;
iii. Kulipa madeni mbalimbali yaliyohakikiwa na Serikali;
iv. Kuhakikisha kuwa ununuzi wa umma unawiana na thamani ya fedha itakayotumika; na
v. Kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma ili zitumike kama ilivyokusudiwa.

# 4. MABORESHO YA MIFUMO YA KODI, ADA NA TOZO MBALIMBALI

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imefanya maboresho mbalimbali kwenye mifumo ya kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali za kodi ili kuongeza mapato, kuongeza ajira na kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi. Baadhi ya maboresho hayo ni kama yafuatayo;

**a. Marekebisho katika Sheria ya Ongezeko la thamani (VAT), SURA 148** kwa:

- Kutoa **msamaha** wa VAT kwenye :
  - **Vifungashio** vya madawa ya binadamu kwa ajili ya viwanda vinavyozalisha dawa hapa nchini ili kupunguza gharama za uzalishaji na kulinda viwanda vya dawa vya ndani;
  - **Virutubisho** vinavyotumika kutengenezea vyakula vya mifugo vinavyoagizwa kutoka nje ili kupunguza gharama kwa wafugaji na kuhamasisha ufugaji bora; na
  - **Taulo za kike** (sanitary pads) ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hii muhimu kwa bei nafuu kwa ajili ya kulinda afya ya mama na mtoto wa kike hasa watoto walio shuleni na vijijini.
- Kumpa **Mamlaka** Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa VAT kwa :
  - **Miradi** ya serikali inayotekelezwa kwa **Mikopo ya Kibiashara** ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya Serikali kwa wakati; na
  - **Mikataba** iliyosainiwa baina ya Serikali ya Tanzania na Taasisi za Fedha au Benki ambazo ni Wawakilishi wa Serikali nyingine ambao wamepewa dhamana na Serikali husika kuingia mikataba ya utekelezaji na usimamiaji wa miradi inayogharamiwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo. Lengo ni kuhakikisha kuwa miradi hii inatekelezwa kwa wakati.




**b. Marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya mapato, SURA 332** kwa:

- Kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 20 kwa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya madawa ya binadamu na viwanda vya bidhaa za ngozi ili kuongeza uwekezaji;
- Kumpa mamlaka Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa kodi kwenye miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ya kibiashara ili kutekeleza miradi kwa wakati; na
- Kutoa msamaha wa Kodi ya Zuio inayotozwa kwenye riba kwa mikopo inayotolewa kwa Serikali na Benki, Taasisi za Fedha na Wahisani kutekeleza miradi ya Serikali.

**c. Marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa SURA 147** kwa:

- Kutoweka ongezeko la kodi ya ushuru wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini zisizo za petroli ili kujenga uchumi wa viwanda. Bidhaa hizo zinajumuisha; vinywaji baridi, maji ya matunda, bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini, bia zenye kilevi, vinywaji vikali vinavyozalishwa nchini, sigara zisizo na kichungi na zenye kichungi zinazozalishwa na tumbaku ya hapa nchini.
- Kuongeza ushuru kwenye bidhaa zinazoagizwa nje ya nchi zisizo za petroli ambazo ni pamoja na: Maji ya kunywa ya chupa (kutoka shilingi 61 hadi shilingi 64.05 kwa lita); Maji ya matunda (kutoka shilingi 221 hadi shilingi 232 kwa lita); Bia (kutoka shilingi 765 hadi shilingi 803.25 kwa lita); Bia zisizo na kilevi (kutoka shilingi 561 hadi shilingi 589.05 kwa lita); Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi (kutoka shilingi 2,349 hadi shilingi 2,466 kwa lita); Vinywaji vikali (kutoka shilingi 3,481 hadi shilingi 3,655.05

kwa lita); Sigara (kutoka shilingi 53,235 hadi shilingi 55,896.75 kwa kila sigara elfu moja); Tumbaku iliyo tayari kutengeneza sigara (kutoka shilingi 26,888 hadi shilingi 28,232.4 kwa kilo).

- ⇨ Kuanzisha Ushuru wa Bidhaa wa shilingi 200 kwa lita kwenye mvinyo uliotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda (kama ndizi, rozela/choya, nyanya, nk) yanayozalishwa hapa nchini tofauti na zabibu kwa kiwango kinachozidi asilimia 75.
- ⇨ Kuanzisha Mfumo Mpya wa Stempu za Kodi za Kielektroniki kwenye bidhaa zinazozalishwa viwandani ili kupata taarifa sahihi za uzalishaji kwenye zitakazosaidia mipango mbalimbali ya kitaifa.

**d. Marekebisho ya sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290** kwa;

- ⇨ Kumpa **mamlaka** Waziri wa Serikali za Mitaa kuzitaka Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya fedha wanazokusanya kutokana na vyanzo vyao vya Mapato kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya Vijana (asilimia 4), Wanawake (asilimia 4) na watu wanaoishi na ulemavu (asilimia 2)
- ⇨ Kuzitaka Taasisi/Makampuni kulipa Ushuru wa Huduma na Mazao.

**e. Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi SURA 438** kwa; kuanzisha utaratibu maalumu wa kusamehe Kodi ambao unalenga kusamehe malimbikizo ya **Riba na Adhabu** kwa (asilimia 100) kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai 2018 hadi 31 Disemba 2018 ili kuwezesha Serikali kukusanya malimbikizo ya madeni ya Kodi.

**f. Marekebisho kwenye Sheria zifuatazo; Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, SURA 290; Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348; Sheria ya Benki Kuu, SURA 197,** ili kuanzisha Akaunti Jumuifu ya Hazina itakayotumika kupokea fedha zote za Serikali na kufanya malipo yote ya Serikali, kwa lengo la kurahisisha usimamizi wa fedha za umma.

**g. Marekebisho kwenye Sheria zinazosimamia Bodi za Mazao mbalimbali** kwa lengo la kuwezesha **ushuru** wote unaokusanywa na Bodi hizo kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, ili kuhakikisha mapato yatokanayo na Ushuru unaotozwa kwenye mazao mbalimbali yanasimamiwa ipasavyo na kutumika kwenye shughuli zilizokusudiwa.

**h. Marekebisho ya viwango vya Ada na Tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa Uchumi** ikiwa ni pamoja na ;-

- ⇨ Kusamehe Kodi ya Ardhi kwa Taasisi za Serikali zinazotoa huduma;
- ⇨ Kufuta na kupunguza baadhi ya viwango vya Tozo na Ada zinazotozwa kwenye sekta ya uzalishaji wa Chumvi ili kupunguza gharama na kuvutia wawekezaji;
- ⇨ Kurekebisha Ada na Tozo zinazotozwa na Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA).

i. **Marekebisho yamefanyika pia kwenye: Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004; Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41; pamoja na Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya sheria za kodi na sheria nyingine mbalimbali;** ili kuwezesha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/19 kama ilivyopangwa.




# 5. NAMNA SERIKALI ITAKAVYOPATA MAPATO

Fedha za kugharamia matumizi ya Serikali hupatikana kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo ni **mapato ya ndani, misaada na mikopo**. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Serikali inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 32,476.0** ili zitumike kugharamia bajeti. Mchanganuo wa vyanzo ni kama ufuatao;

a. **Mapato ya ndani** yenye jumla ya **shilingi bilioni 20,894.6** yakijumuisha:

i. ***Shilingi billioni 18,000.2*** kutoka kwenye ***kodi*** ikijumuisha; *kodi ya mapato* (kutokana na mishahara, vipato vya watu binafsi na makampuni); *Kodi ya Ongezeko la Thamani* na Ushuru wa bidhaa (kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma); na *Ushuru wa forodha na bidhaa zinazouzwa nje* (kwenye uagizaji na usafirishaji wa bidhaa nje).

ii. ***Shilingi bilioni 2,158.8*** kutoka kwenye **mapato yasiyo ya kodi** ikijumuisha; faini, ada, na uuzaji wa nyaraka za zabuni; na

iii. ***Shilingi bilioni 735.6*** zinazotokana na mapato ya Halmashauri.

b. **Misaada na mikopo nafuu** yenye jumla ya **shilingi bilioni 2,676.6** ikijumuisha Shilingi bilioni 545.8 (Misaada ya kibajeti), Shilingi bilioni 2,005.0 (Misaada na mikopo nafuu ya miradi), na Shilingi bilioni 125.9 (Misaada na mikopo nafuu ya kisekta).

c. **Mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara yenye** jumla ya **Shilingi bilioni 8,904.7** ikijumuisha; Shilingi billioni 3,111.0 (mikopo ya *nje*), na Shilingi bilioni 5,793.7 (*mikopo ya ndani*).




# 6. JINSI SERIKALI INAVYOTARAJIA KUTUMIA MAPATO

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imepanga kutumia **Shilingi bilioni 32,476.0** katika maeneo makuu mawili ya kibajeti kwa mgawanyo ufuatao:

a. **Shilingi bilioni 20,468.7 (**asilimia 63 ya bajeti yote) ni **Matumizi ya Kawaida** yatakayo gharamia shughuli za uendeshaji wa Serikali. Hii inajumuisha *shilingi bilioni 7,410.0* za mishahara*; shilingi bilioni 10,004.5* kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali na michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; na Shilingi *bilioni 3,054.2* kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi pamoja na kutoa huduma nyinginezo katika jamii.


b. **Shilingi bilioni 12,007.3** sawa na asilimia 37 ya bajeti yote ni **Matumizi ya Maendeleo**, ambapo shilingi bilioni 9,876.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,130.9 ni fedha za nje. Matumizi ya maendeleo yatatumika kugharamia miradi mbalimbali ya

maendeleo kama vile ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha kimataifa, Ujenzi wa barabara za kuunganisha mikoa na zile za vijijini, Uimarishaji wa usafiri wa anga na majini, Ujenzi wa hospitali, shule, miundombinu ya maji n.k.

### Upelekaji wa Ruzuku kwenda Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Kwa mwaka wa fedha 2018/19 Serikali inatarajia kupeleka ruzuku ya jumla ya **shilingi bilioni 5,206.8** kwenda Mamlaka ya Serikali za Mitaa zote nchini. Kati ya fedha hizo *shilingi bilioni 4,133.1* ni matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 3,942.7 ni mishahara na *shilingi bilioni 190.3* ni matumizi mengineyo. Ruzuku ya fedha za maendeleo inatarajiwa kuwa *shilingi bilioni 1,073.9.* Mchanganuo wa ruzuku kisekta kwenye Serikali za Mitaa ni kama ufuatavyo: -

- Sekta ya elimu shilingi bilioni 3,211.5;
- Sekta ya afya shilingi bilioni 835.6;
- Sekta ya kilimo shilingi bilioni 139.4;
- Sekta ya barabara shilingi bilioni 34.9;
- Sekta ya maji shilingi bilioni 153.6; na
- Sekta ya utawala shilingi bilioni 660.3.
- Ruzuku kwa ajili ya miradi ya kuongeza mapato katika Halmashauri shilingi bilioni 171.5




Vilevile, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatarajiwa kukusanya na kutumia fedha jumla ya **shilingi bilioni 735.5** ambapo *shilingi bilioni 389.8* ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na *shilingi bilioni 345.7* ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

## Mipango na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2018/19 kwa nchi nzima

Muhtasari wa mipango na matumizi ya mwaka 2018/19 kwenye programu, miradi na shughuli mbalimbali kwenye baadhi ya sekta kwa nchi nzima ni kama ifuatavyo:

### Viwanda, Biashara na Uwekezaji

Katika mwaka wa fedha 2018/19 sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imetengewa jumla ya **shilingi bilioni 143.3**. Ili kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya uchumi wa viwanda inatekelezeka kama ilivyopangwa Serikali imepanga kufanya tathmini ya hali halisi ya uzalishaji viwandani pamoja na mahitaji ya bidhaa za viwanda hususani vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini zinazotokana na kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, shughuli nyingine muhimu zitakazofanyika ni kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya viwanda; kuendelea na utekelezaji wa mikakati mikuu ya kuendeleza sekta za alizeti, ngozi na bidhaa za ngozi, pamba mpaka mavazi, na viwanda vya dawa; kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda hususani viwanda vidogo na vya kati na biashara ndogo nchini. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 11.8** kwa ajili ya kuendeleza viwanda vidogo ikiwa ni pamoja na kujenga maeneo ya viwanda katika mikoa ya Manyara, Mtwara, Dodoma, Kagera, Njombe, Katavi, Geita na Simiyu;
ii. **Shilingi bilioni 11.0** kwa ajili ya kuendeleza eneo la viwanda vya nguo TAMCO ikiwa ni pamoja na kujenga mtandao wa barabara eneo la mradi;
iii. **Shilingi bilioni 10.0** kwa ajili ya kuendeleza tafiti za maendeleo ya viwanda katika taasisi za TIRDO, TEMDO na CAMARTEC;
iv. **Shilingi bilioni 22.7** kwa ajili ya Kukamilisha malipo ya fidia katika maeneo ya SEZ yaliyotengwa (Tanga, Kigoma, Ruvuma na Manyoni) pamoja na uanzishwaji wa vituo vya biashara vya Kurasini na Kigamboni;
v. **Shilingi bilioni 2.0** kwa ajili ya kiwanda cha kuunganisha matrekta aina ya URSUS – TAMCO, Kibaha;
**vi.** **Shilingi bilioni 2.0** kwa ajili ya kulipa fidia kwenye Mradi wa Magadi Soda – Engaruka;
vii. **Shilingi bilioni 10** kwa ajili ya kuendeleza miradi ya makaa ya mawe Mchuchuma na Linganga katika mkoa wa Njombe;
viii. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya ujenzi wa Kongani la Viwanda vya Ngozi na Bidhaa za Ngozi mkoani Dodoma; na
ix. **Shilingi bilioni 0.2** kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kufufua Kiwanda cha Matairi cha General Tyre – Arusha.

## Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni Sekta inayoajiri watu wengi zaidi hasa katika maeneo ya vijijini. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 606.8** kwa ajili ya Sekta hii. Baadhi ya matumizi ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 156.9** kwa ajili ya maboresho ya huduma za kilimo, mifugo na uvuvi katika Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
ii. **Shilingi bilioni 40.8** kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Ngono na Bwawa la Kalebe-Kagera;
iii. **Shilingi bilioni 15.0** kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula nchini;
iv. **Shilingi bilioni 14.0** kwa ajili ya ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa;
v. **Shilingi bilioni 11.0** kwa ajili ya pembejeo, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 10.0 ni za madawa ya mimea na kudhibiti milipuko ya wadudu na shilingi bilioni 1.0 ni za kuendeleza mifumo ya uzalishaji wa mbegu;
vi. **Shilingi bilioni 9.3** kwa ajili ya Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Mpunga;
vii. **Shilingi bilioni 9.0** kwa ajili ya ununuzi wa mahindi kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko;
viii. **Shilingi bilioni 11.5** kwa ajili ya ukarabati wa Vyuo vya Kilimo, Vituo vya Wakulima, Ofisi za Kitengo kipya cha Intelijensia ya Masoko na Vyuo vya Mafunzo kwa Maofisa Ugani na Vituo vya Utafiti wa Kilimo;
ix. **Shilingi bilioni 4.8** kwa ajili ya mradi wa kudhibiti *Sumukuvu* nchini; na
x. **Shilingi bilioni 1.2** kwa ajili ya kuchangia Sensa ya Kilimo itakayofanyika nchi nzima.

## Elimu

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 4,641.5** kwa ajili ya Sekta ya Elimu. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kutoa Elimu Msingi Bila Ada; Kutekeleza miradi ya maendeleo ya elimu kupita programu mbalimbali; na Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kuboresha miundombinu ya elimu. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 285.93** zimetengwa katika bajeti za mikoa yote nchini kwa ajili ya kuendelea kugharamia *Elimu Msingi Bila Ada*;
ii. **Shilingi bilioni 114.1** kwa ajili ya uendeshaji wa mitihani ya kitaifa ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu nchi nzima;

iii. **Shilingi bilioni 107.0** zimeelekezwa katika vyuo vya ufundi stadi nchini ili kuboresha miundombinu na kuimarisha huduma zinazotolewa na vyuo hivyo;
iv. **Shilingi bilioni 65.3** zitatumika kuboresha miundombinu ya vyuo vikuu nchini ikiwemo ukarabati, upanuzi na uendeshaji wa vyuo hivyo.
v. **Shilingi bilioni 427.5** zitatumika kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu;
vi. **Shilingi bilioni 142.20** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya elimu kupitia programu mbalimbali; na
vii. **Shilingi bilioni 26.51** kwa ajili ya masuala ya utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu.

## Afya

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 1,731.8** kwa ajili ya Sekta ya Afya kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini. Pamoja na mambo mengine, Serikali itaendelea kuimarisha: huduma ya chanjo kwa watoto, kinga dhidi ya magonjwa yanayotokana na kutozingatia usafi; huduma za magonjwa yasiyoambukiza; huduma ya afya ya uzazi na mtoto; kupunguza maambukizi ya Malaria, TB na VVU/UKIMWI; upatikanaji wa dawa; ubora wa huduma zinazotolewa katika vituo vya afya; na upatikanaji wa damu salama. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 22.9** kwa ajili ya posho ya madaktari wa mafunzo kwa vitendo;
ii. **Shilingi bilioni 12.2** kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika maeneo yaliyobainika kuwa na changamoto za utoaji huduma ambapo lengo kuu ni kupunguza vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi;
iii. **Shilingi bilioni 11.2** kwa ajili ya matengenezo ya vifaa tiba;
iv. **Shilingi bilioni 34.3** kwa ajili ya uimarishaji wa hospitali za rufaa;
v. **Shilingi bilioni 240** kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi;
vi. **Shilingi bilioni 14.5** kwa ajili ya kuimarisha Taasisi ya Saratani ikijumuisha ununuzi wa mtambo ambao utatumika kufanya uchunguzi wa saratani kwa ufanisi zaidi;
vii. **Shilingi bilioni 20.0** kwa ajili ya kuimarisha Hospitali ya Taifa Muhimbili ili kuiwezesha kuendelea kutoa huduma za kibingwa;
viii. **Shilingi bilioni 23.8** kwa ajili uendeshaji wa hospitali za mikoa; na
ix. **Shilingi bilioni 33.0** kwa ajili ya udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza.




## Maji

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali inalenga kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama; Usafi wa mazingira vijijini na mijini; Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; Uendelezaji wa huduma ya umwagiliaji; na Utekelezaji wa masuala mtambuka. Serikali imetenga **shilingi bilioni 859.2** kwa ajili ya Sekta ya Maji, ambapo mchanganuo wa matumizi ya baadhi ya maeneo ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 353.8** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini;
ii. **Shilingi bilioni 176.4** kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa 18 na wilaya 35;
iii. **Shilingi bilioni 62.5** kwa ajili ya kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira jijini Dar es salaam;
iv. **Shilingi bilioni 23.0** kwa ajili ya mradi wa maji Ziwa Victoria - Kahama/Shinyanga;
v. **Shilingi bilioni 21.0** kwa ajili ya mradi wa maji Kahama – Nzega –Igunga- Tabora;
vi. **Shilingi bilioni 20.5** kwa ajili ya miradi ya maji kwenye miji mikuu ya Wilaya na miji midogo 50;
vii. **Shilingi bilioni 14.1** kwa ajili ya mradi wa maji wa Kimbiji na Mpera;
viii. **Shilingi bilioni 12.0** kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa ya Seke Ididi (Shinyanga), Habiya (Simiyu), Matwiga (Mbeya), Manjoro (Simiyu), Looderkes (Manyara), Igumila (Tabora) na Chole/Kwala (Pwani);

ix. **Shilingi bilioni 9.0** kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katika makao makuu ya mikoa mipya 5 (Simiyu, Geita, Katavi, Njome, na Songwe); na
x. **Shililingi bilioni 5.9** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa ya Kidete (Morogoro), Wanging'ombe (Njombe), Nsekwa (Katavi), Dongo (Manyara), Kisangaji (Dodoma), Nanja (Arusha), Namasogo (Mtwara) na Mianjo (Singida);

## Usafirishaji

Katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda nchini, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika uwekezaji wa miundombinu wezeshi ya kiuchumi katika usafirishaji ambayo ni barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege. Ili kuimarisha miundombinu katika sekta ya usafirishaji, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 4,524.2**. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 1,500** kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa (Dar es Salaam – Morogoro , Morogoro – Makutopora na Isaka – Rusumo);
ii. **Shilingi bilioni 252.6** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli kupitia Mfuko wa Reli;
iii. **Shilingi bilioni 495.6** kwa ajili ya ununuzi wa ndege mpya na uimarishaji wa Shirika la Ndege la Taifa (ATCL);
iv. **Shilingi bilioni 20.0** kwa ajili ya ununuzi wa rada pamoja na kuimarisha miundombinu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa;
v. **Shilingi bilioni 20.0** kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa meli katika maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria;
vi. **Shilingi bilioni 6.0** kwa ajili ya usimikaji wa vifaa na miundombinu ya ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege nchini;
vii. **Shilingi bilioni 15.0** kwa ajili ya kuimarisha anuani za makazi, ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano, ujenzi wa kituo cha kutengeneza vifaa vya TEHAMA;
viii. **Shilingi bilioni 215.0** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini ikijumuisha ujenzi wa viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Kigoma, Msalato, Mpanda, Sumbawanga, Tabora, Shinyanga, Songwe pamoja na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Mwanza, Arusha, Mtwara na Kilimanjaro;
ix. **Shilingi bilioni 9.1** kwa ajili ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa vivuko pamoja na upanuzi wa maegesho ya vivuko maeneo mbalimbali nchini;
x. **Shilingi bilioni 567.6** kwa ajili ya matengezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani nchini;
xi. **Shilingi bilioni 272.6** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za mijini na vijijini kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA).

xii. **Shilingi bilioni 961.9** kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami km 597.10 nchi nzima, ujenzi wa madaraja 15 na ukarabati wa barabara za lami km 72.10 kupitia Wakala wa Taifa wa Barabara (TANROADS).

xiii. **Shilingi bilioni 549.1** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, ukarabati wa magati ya bandari za ziwa Victoria, Nyasa na Rukwa pamoja na ujenzi wa bandari kavu katika eneo la Ruvu, mkoa wa Pwani.

## Nishati

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 1,702.3** kwenye Sekta ya Nishati. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na: Kuongeza ufuaji wa umeme; Kuimarisha mifumo ya usafirishaji wa umeme mkubwa nchini; Kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA III); Kuendelea na ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Kuimarisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; na Kuendeleza miradi ya nishati jadidifu (jotoardhi, upepo na umeme-jua). Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 43.6** kuendeleza rasilimali ya jotoardhi, utakaohusisha uchorongaji wa visima vya utafiti na kufanya tafiti ili kuanza kuzalisha umeme unaotokana na jotoardhi;

ii. **Shilingi bilioni 11.1** zimetengwa kugharamia uboreshaji mifumo ya gridi, upatikanaji wa huduma ya umeme pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati jadilifu;

iii. **Shilingi bilioni 412.1** kwa ajili ya usambazaji wa umeme vijijini na makao makuu ya wilaya nchini;

iv. **Shilingi bilioni 13.0** zimetengwa kugharamia ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 220, Makambako-Madaba-Songea;

v. **Shilingi bilioni 80.3** kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 400, Rufiji-Chalinze-Dodoma na upanuzi wa vituo vikuu vya kupoza umeme wa gridi kV 400/220 katika Miji ya Chalinze na Dodoma;

vi. **Shilingi bilioni 12.0** kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa mitambo ya MW 240, Kinyerezi II kwa kutumia gesi asilia;

vii. **Shilingi bilioni 164.0** zimetengwa kugharamia upanuzi wa mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi I ili kuweza kuzalisha MW 185 zaidi;

viii. **Shilingi bilioni 44.8** kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa KV 400, Sumbawanga – Mpanda -Kigoma – Nyakanazi;

ix. **Shilingi bilioni 47.8** kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 400, Dar es Salaam (Kinyerezi)-Chalinze-Arusha; njia za umeme za msongo wa kV 220, Segera-Tanga na Kibaha-Bagamoyo; na kujenga vituo vya kupozea umeme Chalinze, Segera, Bagamoyo na Tanga;

x. **Shilingi bilioni 0.7** zimetengwa kugharamia maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa MW 2,100 kwa kutumia maji ya Mto Rufiji, eneo la ***Stiegler's Gorge*** ili
xi. **Shilingi bilioni 4.3** zimetengwa kugharamia ujenzi wa mitambo ya kufua umeme MW 45 kwa kutumia maji ya mto Malagarasi;
xii. **Shilingi bilioni 15.0** kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme ya Singida-Arusha-Namanga na ujenzi wa kituo kipya cha kupozea umeme Kisongo (Arusha);
xiii. **Shilingi bilioni 32.2** ili kugharamia ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Dodoma na Dar es Salaam;
xiv. **Shilingi bilioni 54.2** kwa ajili ya ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Kabaale (Uganda) hadi Tanga, kupitia Kagera, Geita, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara hadi Bandari ya Tanga.

## Madini

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 1,497.6** kwa ajili ya Sekta ya Madini. Lengo ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini; Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; na Kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika miradi ya kimkakati ya Sekta ya Madini. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 9.1** kwa ajili ya Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini na uendelezaji wa sekta ndogo ya madini ikijumuisha uanzishaji wa kituo cha maonesho ya madini;



ii. **Shilingi bilioni 8.6** kwa ajili ya kuendeleza Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira pamoja na ujenzi wa Mtambo wa Kufua Umeme wa MW 200; na
iii. **Shilingi bilioni 1.8** kwa ajili ya Mradi wa kutoa taarifa mbalimbali za ukusanyaji na matumizi ya mapato yatokanayo na rasilimali za madini.

## Ardhi

Katika mwaka wa fedha 2018/19 Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 73.1** kwa ajili ya Sekta ya Ardhi. Mkazo mkubwa utakuwa ni kuimarisha huduma za Sekta ya Ardhi katika ngazi za Mikoa na Halmashauri zote nchini; Kuhakikisha kunakuwa na uhakika wa milki za ardhi na kurahisisha umiliki wa ardhi; Kuongeza mchango wa Sekta ya Ardhi katika uchumi; na Kuhakikisha kuwa ardhi inatumika kwa tija na kuwa na makazi bora na endelevu. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 5.0** kwa ajili ya Miradi ya Mipango ya Matumizi ya ardhi;
ii. **Shilingi bilioni 8.0** kwa ajili ya Mpango wa Ufuatiliaji na udhibiti wa Ardhi;
iii. **Shilingi bilioni 1.1** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Serikali;
iv. **Shilingi bilioni 2.3** kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka ya kimataifa;
v. **Shilingi bilioni 0.5** kwa ajili ya ukuzaji wa teknolojia ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu;
vi. **Shilingi bilioni 12.0** kwa ajili ya program ya **kuwezesha** umilikishaji wa ardhi; na
vii. **Shilingi 1.5 kwa** ajili ya program ya kuboresha ustawi wa ardhi.

## Ukuzaji wa Ajira na Uendelezaji wa Ujuzi.

Serikali kupitia Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2018 imeweka mkazo mkubwa katika kuongeza fursa za ajira kwa kuweka mazingira wezeshi kwa wadau wote wa Sekta ya Umma na Binafsi katika kushiriki kikamilifu kwenye uendelezaji wa rasilimali watu. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 470.0** ili kufanikisha lengo hilo. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni pamoja na:


i. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kutoa mikopo yenye masharti nafuu;
ii. **Shilingi bilioni 15** kwa ajili ya kuwezesha Programu ya Kukuza Ujuzi na Kuongeza Fursa za Ajira na Kazi zenye Staha ikiwa ni pamoja na kukuza ujuzi kwa Waajiriwa 500 katika sekta za kipaumbele; Kuwezesha wahitimu 2000 kufanya mafunzo mahala pa kazi; na Kutoa mafunzo kwa wanagenzi 4,000 kwa kupitia taasisi za mafunzo na waajiri;
iii. **Shilingi bilioni 305.6** zimetengwa kugharamia ajira mpya 54,209 kwenye sekta ya umma; na

iv. **Shilingi bilioni 73.5** ikiwa ni asilimia 10 ya mapato yanayokusanywa kutoka vyanzo vya Halmashauri zimetengwa kwa ajili ya vijana, wanawake, wazee na walemavu katika ngazi ya Serikali za Mitaa

## Hifadhi ya Jamii

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 978.4** kwa ajili ya kuwezesha makundi mbalimbali kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo pamoja na shughuli mbalimbali za kijamii. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 946.2** kwa ajili ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Fedha hizi zitatumika kulipa stahili za wastaafu pamoja na matibabu kwa wafanyakazi na wategemezi wao;
ii. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya upatikanaji wa huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza na watoto walio katika mazingira hatarishi;
iii. **Shilingi bilioni 0.5** kwa ajili ya Kukarabati makazi ya wazee Bukumbi, Mwanzage na Misufini;
iv. **Shilingi bilioni 0.5** zimetengwa kukamilisha ujenzi wa mahabusu ya watoto Mtwara; na
v. **Shilingi bilioni 1.8** kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa mtoto.



## NYARAKA REJEA ZA BAJETI

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka zinazochapishwa na Serikali na kutumika kama chanzo cha taarifa za kuandaa bajeti:

- Dira ya Maendeleo ya Tanzania, 2025 pamoja na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
- Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 – 2020;
- Mfumo wa Sera za Uchumi Jumla: Unatoa taarifa juu ya sera za bajeti na maboresho;
- Randama za Mipango ya Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati ya mwaka 2018/19;
- Hotuba za Bajeti za Mawaziri za mwaka wa fedha 2018/19;
- Hotuba ya Hali ya Uchumi ya mwaka wa fedha 2018/19;
- Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2018/19;
- Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018;
- Sheria ya Matumizi ya mwaka 2018;
- Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 (Juzuu Na. I – hadi IV).

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo ya nyuma ya vijitabu vya Bajeti Toleo la Mwananchi, uneweza kutembelea mitandao ya:

- Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz)
- Policy Forum (www.policyforum.or.tz)

## ……………(Kwa maoni zaidi kata ukurasa huu)…………………

Je, una mawazo gani, maswali, hisia (unafikiria nini), au una maoni gani kuhusu bajeti hii?

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, unahitaji taarifa zaidi ya hii iliyotolewa katika kijitabu hiki? □NDIYO □HAPANA

Kama ndiyo Je, unahitaji taarifa ya aina gani?

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je kuna kitu kingine zaidi ambacho ungehitaji sisi tukijue?

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, kijitabu hiki kilikusaidia? □ ndiyo □ hapana □ kiasi Fulani

Je kijitabu hiki kilikuwa rahisi kusoma na kueleweka? □ ndiyo □ hapana □ kiasi fulani

**Tuma au fikisha sehemu hii**

Wizara ya Fedha na Mipango-Idara ya Bajeti ya Serikali,
Jengo la Treasury Square,
18 Barabara ya Jakaya Kikwete
40468 Dodoma,
Sanduku la Barua 2802,
**DODODMA-TANZANIA**
Au tuma kwa njia ya barua pepe kwa: ps@mof.go.tz

# Je, Utafanya nini na Taarifa hii?

Bajeti ya taifa ni taswira muhimu ya sura halisi ya kile ambacho Serikali inapanga kufanya kwa mwaka husika. Ukitaka kujua fedha yako ya kodi inakoenda, kama vile mpango wa kuboresha elimu, afya, n.k katika eneo lako, unaweza kuangalia namna na jinsi ambavyo mgawanyo wa fedha unafanyika, hususan kwa ajili ya maendeleo. Kijitabu hiki kinajaribu kutoa muhtasari wa baadhi ya taarifa hizi kwa namna iliyo rahisi kadiri iwezekanavyo. Hata hivyo unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa uandaaji wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo:

- Nyaraka zenye taarifa za bajeti ya Tanzania (***angalia orodha ya nyaraka za rejea***) na hasa, vitabu vinne vya bajeti ya taifa mbavyo vinapatikana katika Wizara ya Fedha (yaani Juzuu Na. I –hadi IV) .
- Wizara ya Fedha na Mipango S.L.P 2802, Dodoma (tovuti http://www.mof.go.tz)
- Ofisi za Halmashauri na/au Maofisa katika eneo lako kama Mwenyekiti Mtendaji wa Kijiji au
- Policy Forum, S.L.P. 38486, Dar es Salaam.

Kumbuka kwamba ni haki yako kujua bajeti hii na taarifa nyingine zinazohusiana na bajeti ya Taifa. Ongea na Viongozi wako kuhusu taarifa hizi na washirikishe watu wengine katika jamii unayoishi nayo.